# LUGHA KAMA KITAMBULISHO: CHANGAMOTO YA "SHENG" NCHINI KENYA

**G.K. King'ei**
*Idara ya Kiswahili na Lugha za Kiafrika, Chuo Kikuu cha Kenyatta*

**Ikisiri**
Makala hii inajadili suala la lugha na utambulishaji wa utamaduni. Inasisitizwa katika makala hii kwamba iwapo lugha itachukuliwa kuwa ni kielelezo na nyenzo ya utamaduni wa kitaifa, basi, katika muktadha wa Kenya ya sasa, kielezo hicho kinatetereka kutokana na hali ya kutatanisha ya lugha nchini humo. Utata huu unadhihirishwa na kuzuka kwa msimbo wa vijana uitwao' "Sheng" ndiko chanzo cha utata huo wa kilugha na kitamaduni, na makala inasisitiza kuwa hali hii ni ishara ya vijana kutokuridhika kitamaduni katika jamii ya kisasa. Makala inamalizia kwa kueleza haja iliyopo ya kuunda upya sera ya kitaifa ya lugha itakayofafanua hadhi na majukumu ya lugha za kigeni kama Kiingereza kwa upande mmoja na Kiswahili na lugha zingine za kiasili kwa upande mwengine.

## 1:0 Utangulizi

Hivi karibuni, masomaji fulani alimwandikia mhariri wa gazeti fulani la kila siku nchini humu barua akilalamikia kushuka kwa kiwango cha ufasaha katika matumizi ya lugha ya Kiswahili. Alishangaa kwa nini lugha hii ambayo ndiyo lugha ya taifa na pia Kiingereza, lugha rasmi zimedharauliwa na kupuuzwa na Wakenya wengi kiasi cha kuzungumzwa kiholela. Analalama kwamba ijapokuwa tumeirithi lugha ya kupendeza ya Kiswahili kutoka kwa wahenga na tunawajibika kuikuza na kuilinda badala ya kuibananga, kile ambacho tutawarithisha wanetu ni kinyume cha kile tulichokirithi kwani tutawapa lugha duni iliyoyumbishwa kwa matumizi yasiyostahili.

Anazidi kulalamika kuwa ingawa ni kweli Kiingereza kinazikalia lugha nyingine zote duniani ikiwemo Kiswahili, pana haja kuu ya kuchunguza hadhi na mahali pa Kiswahili, lugha ambayo ina heshima ya kipekee barani Afrika. Sote tunawajibika kuijenga lugha hii kwani ni muhali na ajabu kuu kwamba tunaionea haya lugha yetu hii ya kitaifa na kimataifa kiasi tunachelea kuitumia. Baadhi ya watu huogopa kudunishwa waizungumzapo ilhali wengine wanaichukia tu moja kwa moja.

Kiini cha barua ya msomaji huyo kilikuwa kwamba hali anayoisimulia hapo juu imepelekea kuzuka kwa msimbo wa mawasiliano ambao ni kama lugha ngeni iitwayo "Sheng". Jina hili limepewa msimbo huo ambao ni kama lugha mseto inayojumuisha Kiswahili na Kiingereza na hata msamiati kutona lugha zinginezo za Kenya. "Sheng" ni kifupisho cha "**Swa**hili-**Eng**lish". Mwandishi wa barua hiyo anatoa mwito wa kubadilishwa kwa mielekeo kuhusu lugha ya Kiswahili pamoja na lugha nyinginezo akisistiza kwamba kila mmoja anao wajibu wa kutekeleza katika juhudi hiyo. Hata hivyo, anafafanua kuwa siyo lazima tuyaue matumizi ya Kiingereza ama lugha zingine ili kukuza Kiswahili (Rono 2001:7)

Maoni ya mwandishi wa barua hiyo, Bwana Rono, yanadhihirisha hali ya kutatanisha ya lugha nchini Kenya kwa sasa. Kwanza kabisa, kwa upande mmoja kuna haja ya kuielewa lugha kuwa sio tu kielelezo cha utamaduni bali hasa kama njia mahsusi ya kuelezea na kusambazia utamaduni wenyewe. Katika maana hii, Kiswahili kimepewa umuhimu mkubwa sana kama nyenzo maalum ya kuelezea utamaduni asilia wa Mwafrika.

Suala la lugha na utambulishaji wa utamaduni linajadiliwa katika makala hii; ns insisitizwa kuwa kama lugha ni kielelezo na nyenzo ya utamaduni wa kitaifa, basi, katika Kenya ya leo, kielezo hicho kinatetereka kutokana na hali ya kutatanisha na labda ya kutetereka pia kwa lugha nchini humu. Utata huu unadhihirishwa na kuzuka kwa msimbo wa vijana uitwao' "Sheng" ambao, kama itakavyoonyeshwa baadaye, ni ishara ya kutoridhika kitamaduni ambako vijana wanahisi katika jamii ya kisasa. Makala inamalizia kwa kueleza haja kuu iliyopo ya kuunda upya sera ya kitaifa ya lugha itakayofafanua hadhi na majukumu ya lugha za kigeni kama Kiingereza kwa upande mmoja na Kiswahili na lugha zingine za kiasili kwa uapande mwengine.

**1.0 Uhusiano wa lugha na utamaduni**

Utamaduni unaweza kuelezwa kwa mapana kuwa ni jumla ya mfumo wa asasi, amali, milekeo, fikira na desturi zinazoitambulisha jamii fulani katika kipindi fulani katika historia. Dhana hii ya utamaduni pia hutumiwa kuelezea jamii ya watu iliyostaarabika, iliyoelimika na illiyoendelea katika vipengele fulani vya maisha. Jamii au kikundi hicho husika sharti kiwe kinatambuliwa na kinajitambulisha kama jamii moja. Mfumo wa imani na fikira unaotokana na utaratibu wa elimu, mafunzo na mila au desturi unaopelekea kukomaa kwa watu wa jamii fulani pia unaweza kuitwa utamaduni. Mwanachuoni maarufu, Taaban Lo liyong, (1972:xi) amefafanua utamaduni kuwa ni, "jumla ya shughuli, kumbukumbu, matumaini, mipango ya baadaye ya jamii fulani zikiwemo pia ndoto na maono yao".

Ni jambo dhaihiri kwamba lugha, ambayo inaweza kuelezwa kama mfumo wa sauti tamkwa zenye maana zinazounganishwa kuambatana na sheria za matumizi na ambazo hutambuliwa na jamii husika, pia ni mfumo unaotumika na kutambuliwa na jamii yenye utamaduni maalum. Hii ina maana kuwa lugha inafungamana sana na ina uhusiano wa karibu na mfumo wa utamaduni wa jamii husika. Kwa ufupi, kauli inaweza kutolewa kwamba utamaduni hugubika asasi zote za kijamii ikiwemo lugha. Hata hivyo, uhusiano kati ya lugha na utamaduni ni jambo lenye utata mkubwa kwani ingawa lugha ni kipengele kimojawapo cha utamaduni, pia ni njia maalum ya kuelezea, kuutetea na kuuhifadhi utamaduni wenyewe. Lugha hueleza utamaduni wa jamii husika katika viwango vyote kama vile tabia, rasilimali, mfumo wa ishara na imani.

Hadi hapa tunaweza kujiuliza, je, ni kwa njia gani ambapo vipengele vya utamaduni kama vile lugha, matabaka na tabia huhusiana katika hali hii ya utata? Kulingana na Fowler (1985:65), lugha sio tu njia ya kujielezea bali pia ni chombo

kinachoashiria tabaka na hadhi ya mtu katika jamii. Kwa hivyo, kutokana na matumizi ya lugha, dini, jinsia, tabaka, umri na maelezo mengine ya mzungumzaji yanaweza kudhihirika. Ni kwa maana hii ndipo inaweza kudaiwa kwamba, msimbo wa "Sheng" unaashiria kitambulisho cha aina fulani kuhusu kiwango cha hadhi na mahali pa mhusika katika jamii yake.

**2.0 Sheng kama tukio la kijamii**

Imeelezwa hapo juu kuwa "Sheng" ni namna ya msimbo au kilahaja cha kundi fulani miongoni mwa vijana. Mfumo huu wa mawasiliano umesanifiwa na vijana, hasa wale wanaoishi katika sehemu za mijini. Mfumo wenyewe hufuata muundo wa kisarufi wa Kiswahili na lugha nyinginezo za kibantu ila hutumia maneno mengi mapya ya kubuniwa na ya mkopo kutokana na lugha mbalimbali kikiwemo Kiingereza. Lugha zinazochangia msamiati wa Sheng ni pamoja na Kikuyu, Kiluo, Kiluhyia, na Kikamba. Maelezo haya ya kijumla kuhusu maana ya Sheng yametolewa na wasomi kadha kama vile Mkangi (1984) ambaye ameueleza msimbo huu kuwa ni lugha mseto au lugha "kiunzi" ya kizazi kipya cha vijana wa mijini.

Kulingana na wachunguzi kadha, Sheng ilizuka katika miaka ya kati kati ya sitini katika sehemu za makazi za mashariki mwa jiji la Nairobi kama vile mitaa ya Kaloleni, Mbotela, Kimathi, Pumwani, Majengo, Bahati, Buruburu, Barma,Umoja, Dandora, Huruma, Mathare, Eastleigh na maeneo yanayoizunguka mitaa hiyo. Kufikia maika ya awali ya 1970, Sheng ilikuwa imepamba moto sio tu jijini Nairobi bali pia katika miji mingine kote nchini Kenya. Kufikia sasa, Sheng imekuwa kitambulisho cha takriban vijana wote nchini, mijini na mashambani wawe wa shuleni au la.

Kulingana na Mukhebi (1986), "Sheng" ni tukio la kitamaduni ambalo lifungamana sana na mawazo au fikira, hisia na matakwa ya msemaji mwake. Anaeleza kuwa wazungumzaji asilia wa Sheng waligundua kuwa kutokana na hali na mazingira yao ya kifukara katika mitaa ya jamii yenye mapato ya chini, hawangeweza kupata elimu yao na kwasiliana kupitia Kiingereza bali walihitaji mfumo wao wenyewe. Anaongezea kuwa kutokana na ufahamu wao duni wa Kiingereza, iliwawia vijana hao muhali kuweza kujifunza masomo mseto kwa Kiingereza kama vile Historia, Jiografia, Fasihi na maisha ya kijamii ya Waingereza, masomo yaliyokuwa ya kimsingi katika mitaala ya shule za msingi wakati huo.

Je, msimbo huu wa Sheng iliibuka kutokana na nini? Kufuatia kupatikana kwa uhuru Kenya hapo mwaka wa 1963, idadi ya wakazi wa jiji la Nairobi ilipanda kwa haraka sana kutokana na kumiminika kwa watu kutoka mashambani wakitafuta nafasi za kazi katika mitaa ya viwanda humo jijini. Wananchi hao maskini waliishia kuishi katika mitaa ya makazi duni ya viwandani mashariki mwa Nairobi ambapo ndiko kitovu cha maendeleo ya viwanda. Ijapokuwa wafanyikazi hawa pamoja na jamii zao walilazimika kutumia Kiswahili kwa mawasiliano baina yao, wengi walikichukia Kiswahili kwa vile kilikuwa

kimedunishwa sana na sera ya ukoloni kama lugha ya mashambani, lugha ya vibarua au "maboi" wa kuwatumikia wazungu.
Hata hivyo, watoto wa wafanyikazi hao hawakupendelea kuendelea kukitumia Kiswahili kama wazazi wao kwa sababu kadha. Kwanza kabisa, kinyume na wazazi wao, watoto wale walilazimika kuishi katika hali ya jamii ya utatu-lugha: lugha za kinyumbani, Kiswahili na Kiingereza. Pia, walitambua kuwa ingawa walibidika kutumia lugha nyingi, ni Kiingereza pekee ambacho kilipewa hadhi ya juu kama lugha ya utawala, mamlaka heshima na uwezo wa kiuchumi.

Ili kuepuka matatizo ya kimawasiliano na kama njia ya kusuluhisha utata wa hali hiyo iliyowakabili, vijana hao waliaunda msimbo wa mawasiliano kati yao ambao ingawa ulifuata sarufi ya Kiswahili, uliazima msamiati kutokana na lugha za kiasili na kuunda baadhi ya maneno yake. Msimbo huo ndio uliotokea kuwa Sheng hapo baadaye.

**3.0 Sheng kama kitambulisho miongoni mwa vijana**
Pengine la muhimu zaidi hapa sio kujishughulisha sana na historia au asili ya Sheng lakini kuchunguza hasa ni athari gani ambazo Sheng imekuwa nazo katika hali ya lugha nchini Kenya na pia juu ya jinsi vijana wanavyojielewa ama wanavyojitambulisha. Tumeeleza hapo juu jinsi Sheng ilivyochipuka kutokana na azma ya vijana wa mitaa fulani jijini Nairobi waliokuwa wakijaribu kusuluhisha hali ngumu ya lugha na kijamii walimojikuta. Hata hivyo, ni kweli kwamba msimbo wa Sheng umeanza kuashiria uhalisia mkubwa wa maisha yetu ya kisasa zaidi katika jamii yetu kama Wakenya.

Kulingana na Mkangi (1984), Sheng inaweza kuhesabiwa kuwa kama suluhisho la vijana wa kisasa kwa matatizo ya kisasa ambao wamechukizwa na jamii yao iliyogawika matabaka na hali ya lugha yenye ubaguzi dhidi ya matabaka fulani. Hali hii ya kutatanisha iliibuka kutokana na mfumo ulioanzishwa na wakoloni katika miaka ya mwisho ya karne ya 19 ambao ulikusudiwa kuanzisha, kuendesha na kudumisha jamii yenye matabaka ya kiuchumi. Kielelezo cha matabaka hayo ni kuwepo kwa mitaa ya maskini mashariki mwa jiji na ile ya matajiri magharibi mwake vilevile. Ili kuhakikisha mpangilio huo ulipata mashiko vilivyo, viwanda vyote ambamo maskini na vibarua waliajiriwa, vilipangwa kuwepo katika mitaa ya mashariki, walikoishi wachochole na mafalahi. Mitaa hii ilikuwa na uhaba wa huduma muhimu kama vile shule na hospitali.

Sheng basi, ilichipuka na kustawi kama njia ya mawasiliano kati ya vijana walioishi katika jamii mpya ya kitabaka iliyoundika baada ya majilio ya ukoloni na kuendelea hata baada ya uhuru wa kisiasa mnamo mwaka 1963. Sheng ilikuwa ni ujumbe wa utetezi kwamba vijana hao walifadhaishwa na kughasiwa na mfumo wa jamii yao na pia sera ya lugha ya nchi yao ambayo ilikweza lugha ya kigeni, Kiingereza, juu ya lugha ya taifa, Kiswahili. Vijana wa mitaa ya mashariki mwa Nairobi, waliazimia kuunda "lugha" yao iliyowatambulisha kama Wakenya badala ya lugha zao nyingi tofauti za kinyumbani ambazo waliziona kuwa ni ishara ya "ukabila". Walihitaji lugha ambayo ingekuwa kiungo cha kuwaleta

pamoja kama jamii moja badala ya "makabila" ambayo wakoloni waliyatilia mkazo kama njia ya kuwagawanya Wakenya. Hii ndiyo sababu kuu ya umashuhuri ambao vijana wote nchini wameupa msimbo huu wa Sheng kwani wanaiona Sheng kuwa "lugha" waliyoibuni wao ili kutimiza mahitaji yao maalum. Pengine tunaweza kujiuliza, iwapo vijana hao wahusika walihitaji lugha ya kuwaunganisha, kwa nini hawangeamua kutumia Kiswahili? Jibu ni kwamba ingwa vijana hao hawakukichukia Kiswahili, walikiona kuwa ni lugha duni kutokana athari ya kutwezwa kwa lugha hiyo na wakoloni katika jamii na hasa katika mfumo wa elimu.

**4.0 Sheng kama kifaa cha kijamii**

Ni kweli kwamba Sheng ni tukio muhimu sana katika jamii ya Wakenya hivi leo. Sheng inakubalika miongoni mwa vijana wote kama kitambulisho cha ujana wao na njia ya mawasiliano kati yao licha ya tofati zao za lugha na kijamii na lugha. Msimbo huu si maarufu katika sehmeu za mijini bali nchini kote hasa kati ya vijana waliomo shuleni, vyuoni ama wafanyao kazi pamoja. Sheng inawaunganisha vijana na imekuwa ni ishara maalum inayoonyesha ukiukaji wao wa mipaka ya kitabaka, kijamii na lugha.

Hata hivyo, kwa upande mwingine matumizi ya msimbo wa Sheng yamelaumiwa na waalimu wengi katika shule za msingi na zile za upili kuwa ni sababu mojawapo kuu ya kushuka kwa kiwango cha ujuzi wa lugha ya Kiswahili na Kiingereza miongoni mwa wanafunzi. Sheng imelaumiwa kwamba inasababisha wanafunzi kutozingatia mafunzo ya kanuni za sarufi na tahajia au maendelezo. Kwa hakika ni msimbo ambao hauzingatii sheria za sarufi na tahajia kwa sababu zisizofahamika kwani ingawa muundo wake wa kisarufi ni ule wa Kiswahili, Sheng hupuuza sarufi ya Kiswahili katika matumizi yake.

Kwa maoni ya baadhi ya wataalam wa lugha, msimbo wa Sheng ni kama vile juhudi za aina hiyo zinazofanywa na baadhi ya watumiaji wa lugha ya Kiingereza ambao wamekuwa wakijaribu kuifanya lugha hiyo kuwa kama ya "Kiafrika". Mifano ya matumizi kama hayo ya Kiingereza yametolewa na Nnamonu (1985) ambaye amedai kuwa mengi ya matumizi kama hayo huwa ni makosa yasiyokusudiwa na yanayotokana na athari za lugha za kiasili za Kiafrika. Kwa Mfano: *Accommodations, Advices, Ammunitions, Beards, Behaviours, Cutleries, Damages, Funs, Equipments, Elites, Furnitures, Gossips, Luggages, Machineries, Offsprings, Staffs, na Stationeries.*

Vilevile, maneno ya majina yafuatayo hutumika kimakosa kwa kutangulizia kibainishi **:a,** kwa mfano**:** *A advice, A help, A harm, A permission na A treatment*.

**6.0 Muundo wa Sheng**

**6.1 Uundaji wa Majina**

Gichagi *(rural area)* (Gikuyu)

| | | |
|---|---|---|
| Moti | *(motor-car)* | Kiingereza |
| Chapa | *(money)* | Kiingereza |
| Sosi | *(eat)* | (Neno jipya) |
| Budaa | *(father)* | (Neno jipya) |
| Hao | *(house)* | (Kiingereza) |

### 6.2 Uundaji wa Vitenzi

Baadhi ya vitenzi huundwa kwa kuunganisha mwanzo ku na mzizi kwa kitenzi mkopo kutokana na lugha nyingine za Kenya au vitenzi vipya vya kubuniwa vilivyopewa kimabishi cha mwisho cha Kiswahili. Mifano:

| | |
|---|---|
| Ku-ushi | (kuondoka, kwenda au kutoweka). |
| Ku-noki | ( kukasirika) kutokana na neno la Kiingereza "knock". |
| Ku-sare | ( kupeana bila malipo: Kiingereza, "surrender") |
| Ku-wea | ( kuvaa: Kiingereza "wear") |

### 6.3 Ufupishaji

Tao (town)
Mat (matatu)

### 6.4 Maendelezo ya Majina

Ili kuyapa maneno ya majina, Sheng huunda majina yenye kuanza na kiambishi awali **"o"**- kuunda majina halisi ya mahali na watu kwa kutumia viambishi tamati "-shi". Mifano:

| | |
|---|---|
| Odhiambo | Odhishi |
| Mutunga | Mutushi |
| Kilonzo | Kiloshi |
| Makokha | Makoshi |
| Nairobi | Nairoshi |
| Namanga | Namashi |

### 6.5 Mundo wa Sentensi

Kama ilivyodokezwa hapo juu, sentensi katika msimbo wa Sheng hufuata sarufi ya lugha za Kibantu na hasa Kiswahili. Kwa mfano:

***Amedinda***" (Amekataa). Hapa **a** ni kiima, **me** ni wakati, **kataa** ni kitenzi. Kwa hivyo, ni dhahiri kwamba Sheng ni jitihada za kuunda msimbo wa mawasiliano ambao ni kama lugha-mseto kati ya Kiswahili na Kiingereza. Kwa hakika, kama tulivyokwishakugusia, Sheng inafuata sarufi ya Kiswahili na kutumia maneno ya Kiingereza na lugha nyinginezo za Kikenya. Utaratibu huu, kwa maoni ya baadhi ya wataalamu, muundo wa Sheng hutinga juhudi za kufunza lahaja rasmi yaani Kiswahili na Kiingereza sanifu. (Kiama 1990, Asiba 1985, na Ochieng 1990).

**Hitimisho**

Makala hii imedhamiria kufafanua kwa ufupi asili na sababu za kuzuka kwa msimbo wa Sheng kama kifaa cha kutosheleza mahitaji fulani ya lugha na kijamii ya vijana wa sehemu za mijini katika miaka ya sitini na sabini. Msimbo huu umeonyeshwa kuwa ishara ya kuambaa uzingatiaji wa lugha sanifu ya Kiswahili na Kiingereza. Pia Sheng inaweza kuhesabika kuwa juhudi ya vijana wa kizazi kipya ya kuua "ukabila" kwa kushirikisha maneno ya lugha tofauti pamoja na kuunda msamiati wa kipekee katika msimbo wa Sheng.

Jambo muhimu kabisa ni kwamba Sheng imeonyeshwa kuwa ni njia ya mawasiliano na kitambulisho cha kijamii kwa vijana wa matabaka ya chini katika mitaa ya kimaskini ya mashariki mwa Nairobi ambayo ilikua na kuenea hadi kugubika sehemu zote za Jamhuri ya Kenya kutoka mijini hadi mashambani. Makala imejaribu kuonyesha jinsi vipengele vya lugha na utamaduni vinavyochangiana na kuathiriana kwa kutumia mfano wa kuzuka na kusambaa kwa Sheng nchini Kenya. Kama vile Mazrui na Mazrui (1995) wanavyodokeza, mabadiliko ya lugha ni ushahidi wa mabadiliko mapana zaidi katika mfumo wa utamaduni unaohusika. Kuzuka kwa Sheng katika miaka ya kumeonyeshwa kama kulitokana na kutoridhika kwa vijana walioishi katika mitaa ya matabaka ya chini na hali ya lugha pamoja na sera yake.

Hali ya kutatanisha ya lugha iliyowakabili vijana hawa ni ile iliyosababishwa na sera ya lugha ya kikoloni iliyorithishwa Wakenya na Waingereza. Katika sera hii, lugha za kwanza hazikutumiwa katika shule za sehemu za mjini ambapo Kiingereza kilitumika huku Kiswahili kikiwa kama lugha ya tabaka la chini na kikinyimwa nafasi katika mfumo wa elimu. Kwa vile vijana waliohusika walizaliwa mijini au mashambani, wengi wao walichukia kufunzwa kwa Kiingereza, lugha ambayo hawakuitumia nyumbani au katika maisha yao ya kila siku. Hii inamaanisha wangeridhika zaidi kama wangelifunzwa kwa lugha zao za kwanza au kwa Kiswahili. Kwa hivyo, walitunga "lugha" yao ya Sheng anbayo waliitumia ili kujitofautisha na vijana wa matabaka ya juu waliobobea katika lugha na utamaduni wa Kiingereza na ambao walichukia Kiswahili na lugha za kiasili.

Ingawa Kiswahili kimeanza kutumiwa kufunzia shule za mijini na kufanywa somo la lazima katika mfumo wa elimu ya msingi na upili, bado ushindani na mvutano upo baina ya lugha hizi. Pengine njia ya pekee ya kulitatua tatizo hili ni kuikweza lugha ya Kiswahili na kuwa na taifa lenye lugha mbili rasmi, Kiswahili na Kiingereza. Hatua kama hiyo ingesaidia kuondoa mtafaruku wa lugha katika viwango vya kijamii, kielemu, siasa, uchumi na biashara na ungeipa lugha ya Kiswahili hadhi inayostahiki kama lugha ya kitaifa.

Kwa kumalizia, tunapaswa kujiuliza maswali yafuatayo:

- Je, kwa vile Sheng imeenea sana miongoni mwa vijana wa Kenya ambao ni aslimia 60% ya Wakenya wote, tunaweza kuujenga na kuuendelza msimbo

huo kuwa “lugha” kamili ya mawasiliano na hata kuitungia vitabu badala ya kuikashifu na kuipinga? Bila shaka, kwa sasa jibu la swali hili ni la hatuwezi kwa vile Sheng sio lahaja ya lugha yoyote inayojulikana ila ni msimbo tu miongoni mwa vijana. Lakini, iwapo hilo ni kweli, sharti tujiulize, je, tutafanya nini kuhusu vizazi vingi vya jamii maskini vinavyozaliwa mijini kwenye mitaa au mabanda na ambavyo vinategemea tu Sheng wala havina nafasi ya kujifunza lugha au lahaja rasmi?

- Mbinu gani za kufunzia lugha zinafaa kutumiwa ili kupunguza makali ya athari za lugha za mitaani za vijana kama vile msimbo wa Sheng juu ya lugha au lahaja rasmi ya Kiswahili au Kiingereza?

- Kwa vile hali na sera ya lugha nchini Kenya ni kielelezo cha hali ilivyo katika mataifa mengi ya Kiafrika na pia katika mataifa yanayostawi, ni kwa njia gani upangaji wa lugha unaweza kushirikisha vipengele vya utamaduni na maisha ya kijamii kwa jumla ili kuyapa maswala ya kitamaduni kipaumbele katika ustawishaji wa lugha?

Maswali haya na mengine yanayoambatana nayo yanafaa kufikiriwa katika upangaji wa mikakati ya maendeleo ya lugha na jamii katika mataifa kama Kenya kwani kuyapuuza maswala yenyewe kutaleta ujenzi wa mifumo chapwa isiyoweza kuridhisha matakwa ya wanajamii wote.

**Marejeo**

Lo Liyong, T. (1972), “Preface” to *The Popular Culture of East Africa,* Nairobi: Longman.

Rono, M. (2001), " We should Arise and Save Kiswahili". *The People*. Nairobi: July 2001 .

Fowler, D. (1987) katika Giglioli, P. (mh.) *Language and the Social Context.* Middlesex: Penguin.

Mazrui, A. na Mazrui, A. (1995). *Swahili, State and Society*. Nairobi. EAEP.

Mkangi, K. (1984), "Sheng and the Kenyan Culture." *The Standard: Nairobi*, August 30.

Nnamonu, J. (1995) *Common Errors in English.* Essex: Longman.

Mukhebi, L. (1986) "Is Language and Culture Inseparable?" *Kenya Times:* Nairobi: May 28.

Ochieng, P. (1990) "Sheng as a Tool Against Tribalism". *Kenya Times.* Nairobi: October 8.

Kiama, B. (1990) "Sheng: Monstrosity or Tool for Unity?" *Kenya Times:* Nairobi: November 12 (11).

Asiba, A. (1985). "Can Sheng Stand the Test of Time?" *Sunday Nation:* Nairobi. August 30, (10).